TANGAZO LA SERIKALI NA. 228 la tarehe 20/3/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA (HIFADHI YA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI YA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hii itaitwa Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lilillo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

Sura ya 191;

"*Baraza*" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"*maeneo ya hifadhi*'' ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Pangani;

"*hifadhi ya mazingira*" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"*madini ya ujenzi*" maana yake ni kokoto, mawe, changarawe, mchanga, chokaa, marumaru, kifusi, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"*mazingira*" maana yake maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi

yanavyoingiliana;

Sura ya 323

"*Mkurugenzi*"maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*misitu*" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu, na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"*mifugo*" maana yake ni Ng'ombe, punda, kondoo, mbuzi, nguruwe, mbwa na mifugo mingine ifugwao na binadamu;

*"ndege" inajumuisha kuku, bata, kanga, njiwa na jamii nyingine ya ndege;*

"*taka*" maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira;

"*taka gesi*" maana yake ni hewa chafu, moshi, joto, au harufu ambayo inaweza kuleta madhara kwa binadamu, mazingira, na viumbe hai wengine;

"*taka ngumu*" maana yake ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara,

viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps);

"*taka yenye madhara*" maana yake ni kitu chochote kigumu, majimaji, cha gesi au taka majimaji ambayo kwa sababu ya athari zake kikemikali, athari kwa mazingira na binadamu, maambukizo yake, kiwango chake cha sumu, ulipukaji na kulika/kubabuka kwake kinadhuru afya, maisha ya binadamu au mazingira;

Sura ya 191

"*taka vimiminika*" maana yake ni taka zilizo katika hali ya maji au vimiminika zitokazo majumbani, kwenye kilimo, maeneo ya biashara au viwandani zilivyofanyiwa au zisivyofanyiwa usafishaji;

"*taka za viwanda*" maana yake ni taka zitokanazo na viwanda vinavyozalisha au visivyozalisha, ambayo ni chanzo cha nishati, maji, mitambo ya kusafisha au mawasiliano;

"*udongo*" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi;

"*vyanzo vya maji*" maana yake ni mahali popote ambapo maji yanapatikana

katika uhalisia wake na panaweza kuwekwa miundombinu ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na viumbe hai wengine.

## SEHEMU YA PILI
## UHIFADHI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira

4. Itakuwa ni Wajibu wa kila mtu, taasisi au asasi yoyote kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kuhakikisha kwamba-

(a) anafanya shughuli zisizoathiri au kusababisha uharibifu au uchafuzi wa mazingira;

(b) anashiriki katika jitihada mbalimbali za utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira; na

(c) anatoa taarifa kwa Halmashauri au mamlaka nyingine husika kuhusu uwepo wa shughuli yoyote inayoathiri au inayoweza kuathiri mazingira au uwepo wa viashiria vya uharibifu wa mazingira.

Jukumu la Halmashauri na Baraza

5. Itakuwa ni jukumu la Halmashauri kwa kushirikiana na Baraza-

(a) kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

(b) kutoa elimu ya usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa mazingira;

(c) kulinda mazingira; na

(d) kuhamasisha umma kushiriki katika masuala ya usimamizi wa mazingira.

Maeneo ya hifadhi

6. (1) Halmashauri itakuwa na jukumu la

kuhakikisha maeneo yaliyohifadhiwa hayavamiwi.

(2) Mtu yeyote, taasisi au asasi inayotaka kufanya shughuli yoyote katika sehemu au maeneo yaliyohifadhiwa ataomba kibali cha Halmashauri.

Siku ya Mazingira

7. (1) Kutakuwa na Siku ya Mazingira ambayo watu wote watashiriki katika uhamasishaji wa shughuli za usimamizi na uhifadhi wa mazingira.

(2) Siku hii inaweza kutumika kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira kwa umma na kutoa tuzo kwa mtu yeyote, taasisi au asasi ambayo imeshiriki vyema katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Halmashauri.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) hapo juu, kila mtu ataendelea kutekeleza wajibu wa kusimamia, kutunza na kuhifadhi mazingira katika maeneo yake.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

8. (1) Kwa lengo la usimamizi wa mazingira Halmashauri itatenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuchimba madini ya ujenzi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito, ndani ya mto, bwawa au katika maeneo yasiyoruhusiwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

Karakana na gereji

9. Matengenezo ya magari, pikipiki au mitambo yatatakiwa kufanyika katika karakana, gereji au maeneo maalumu yaliyoruhusiwa kwa kibali cha Halmashauri.

Uoshaji wa vyombo vya moto

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha gari, pikipiki au mtambo kwenye eneo la barabara, hifadhi ya barabara, njia ya waenda kwa miguu, mtaa, maeneo ya wazi, kando ya mito, maziwa, au kubadilisha matumizi ya eneo lolote ambalo halikutengwa kwa shughuli za aina hizo.

Usimamizi wa mazingira ya machinjio

11. Halmashauri itasimamia maeneo ya machinjio kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika machinjio na kuhakikisha kuwa-

(a) shughuli za machinjio hazichafui mazingira;

(b) eneo lote la kuchinjia limejengwa na kusakafiwa kwa saruji au marumaru;

(c) mifugo inachinjwa katika eneo la kuchinjia;

(d) kuna upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama; na

(e) kumetengwa eneo maalumu la kukusanyia taka zitokanazo na machinjio.

Usimamizi na utunzaji wa fukwe na mialo

12. (1) Halmashauri itawajibika kuweka utaratibu wa kusimamia, kutunza, na kusafisha fukwe au mialo katika maeneo yao.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya shughuli za biashara katika maeneo ya fukwe au mialo bila kibali cha Halmashauri.

(3) Mmiliki wa nyumba au Hoteli iliyo karibu na fukwe au mialo hataruhusiwa kutiririsha maji taka au

kutupa taka ya aina yoyote katika maeneo hayo.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA TAKA

Usimamizi wa taka

13. Halmashauri itaweka utaratibu wa ukusanyaji na utupaji wa taka ambapo-

(a) itatenga maeneo maalumu ya kukusanyia taka; na
(b) itatoa elimu ya uchambuzi wa aina za taka.

Uchambuzi wa taka

14. (1) Ili kutoa nafasi ya usimamizi, usafirishaji na utupaji taka, taka zote zitachambuliwa na kukusanywa kulingana na makundi yafuatayo:

(a) taka zenye madhara au hatarishi;
(b) taka zenye ncha kali;
(c) taka za hospitali; na
(d) taka rejea.

Uhifadhi wa taka za viwandani

15. (1) Kila kiwanda kitakuwa na wajibu wa kutenga na kutumia maeneo maalumu ya kukusanya taka zinazotokana na shughuli za kiwandani.

(2) Kiwanda kinachozalisha taka ngumu, kitahakikisha kwamba taka hizo zinahifadhiwa katika maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili hiyo kabla ya kusafirishwa kwenda kutupwa katika maeneo maalumu.

(3) Kiwanda kinachozalisha taka vimiminika kitahakikisha kwamba taka hizo zinasafishwa ili zisiwe na madhara kwa mazingira na kwa afya na zinahifadhiwa katika maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili hiyo kabla ya kusafirishwa kwenda kutupwa katika maeneo maalumu yaliyotengwa.

Ukaguzi wa viwanda

16. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kukagua viwanda kama vimetenga na kutumia maeneo maalumu ya kukusanya taka kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hii.

Marufuku ya kutiririsha taka vimiminika

17. Itakuwa ni marufuku kutiririsha au kuelekeza maji taka, taka vimiminika au maji ya mvua kutoka viwandani, majumbani, majengo mengine kwenda kwenye vyanzo vya maji, barabarani, ushoroba, mtoni, maeneo ya wazi au sehemu yoyote isiyotengwa kwa ajili hiyo.

Ukusanyaji na uzoaji wa taka

18. (1) Halmashauri itasimamia shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa taka kutoka katika maeneo ya masoko, biashara na maeneo mengineyo zitakusanywa, kuzolewa na kutupwa kulingana na aina ya taka husika.

(2) Shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa taka zinaweza kufanywa na Halmashauri au wakala wake.

Taka za Hospitali

19. Ukusanyaji, usafirishaji na utupaji wa taka za Hospitali na dawa zilizofikia ukomo wa matumizi utafanyika kutokana na taratibu zilizowekwa na Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya.

Udhibiti wa taka gesi

20. (1) Uzalishaji wa taka gesi utadhibitiwa na Halmashauri kwa-

(a) kutenga maeneo maalumu ya ujenzi wa viwanda vinavyozalisha taka gesi; na

(b) kupiga marufuku matumizi ya samadi kama nishati ya kupikia ndani ya nyumba.

(2) Viwanda vya kuzalisha taka gesi vitajengwa katika maeneo yaliyombali na makazi ya watu.

Wachuuzi wa miwa, matunda na mboga mboga

21. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mchuuzi wa miwa, matunda au mbogamboga kuhakikisha kuwa ana

chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya bidhaa.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kufanya biashara ya miwa, matunda au mbogamboga katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Udhibiti wa taka zinazozalishwa kutoka katika vyombo vya usafiri

22. (1) Magari au mabasi yote yanayobeba abiria-

(a) yatapaswa kuweka vyombo maalumu vya kutupia taka zinazozalishwa na kuwataarifu abiria matumizi ya vifaa hivyo; na

(b) yatakusanya na kutupa taka katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kukusanya na uzoaji wa taka katika vituo vya mabasi au kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote akiwa ndani ya gari, basi au chombo chochote cha usafiri kutupa nje kitu chochote.

Chukizo au kero

23. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kujenga kitu chochote kinachoweza kusababisha kero au kilicho katika hali ya uchafu ambacho kinaweza kusababisha-

(a) madhara kwa maisha ya binadamu, wanyama au viumbe hai wengine;

(b) adha, kero, chukizo au kelele kwa watu wengine; na

(c) magonjwa.

Ilani ya kuondoa kero

24. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwepo kwa eneo lenye kero ya aina yoyote atamtaka mmiliki wa eneo husika, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote aliyesababisha kero hiyo kuondoa kero hiyo ndani ya muda utakaoainishwa kwenye Ilani.

(2) Endapo Halmashauri italazimika kuondoa kero, gharama za kuondoa kero husika zitalipwa na mtu aliyesababisha kuwepo kwa kero hiyo.

Utupaji wa taka mbalimbali

25. Wazalishaji wa taka zitokanazo na madawa ya mifugo na kilimo, kemikali, shughuli za kilimo, au aina nyingine yoyote ya taka watakusanya, watazoa na kutupa au kusafirisha taka hizo kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na Halmashauri.

Huduma ya maeneo ya kutupa taka

26.(1) Halmashauri itatenga, itajenga na kuendesha maeneo makuu ya kutupa taka *(Sanitary Landfills)*, maeneo ya kutunza taka kwa muda *(Transfer statations)* na vituo vya kukusanyia taka *(Collection Points)* kabla ya kusafirisha kwenda Dampo Kuu.

(2) Halmashauri inaweza kumpa wakala au kuingia ubia katika kujenga na kuendesha maeneo ya kutupa taka.

Zuio la kufanya shughuli katika madampo

27. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, kampuni au taasisi au kikundi kufanya shughuli yoyote katika maeneo yaliyotengwa kuwa dampo isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri.

Marufuku ya kutupa taka ovyo

28. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, taasisi, au asasi yoyote-

(a) kuzalisha na kutupa taka katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili hiyo;

(b) kutupa taka kwenye mifereji, mitaro, mito, barabara, ufukweni au maeneo ya wazi;

(c) kutiririsha maji taka na taka vimiminika kwenye mifereji, mitaro, mito, barabara, au maeneo ya wazi;

(d) kufanya biashara, maonyesho ya biashara au shughuli nyingine yoyote katika maeneo ya karibu au ndani au juu ya mifereji au mitaro ya maji, au katika maeneo ya kukusanyia taka, au kwenye dampo; na

(e) kuweka mabango au kufanya shughuli yeyote itakayozuia matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA UFUGAJI NA KILIMO

Wajibu wa Halmashauri

29. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya malisho kwa kuzingatia idadi ya mifungo ndani ya Halmashauri;

(b) kutenga njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi kutoka malishoni, kwenye majosho, malambo au mnadani;

(c) kufanya sensa ya mifugo; na

(d) kutoa kadi itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo.

Wajibu wa mfugaji

30. Kila mfugaji atakuwa na wajibu wa kusimamia, kutunza na kuhifadhi mazingira kwa-

(a) kufuga idadi ya mifugo kadri itakavyoamriwa na Halmashauri;

(b) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(c) kupitisha mifugo katika njia *(stock routes)* zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(d) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo;

(e) kufuga idadi maalumu ya mifugo atakayoelekezwa na Halmashauri;

(f) kuchukua tahadhari zote muhimu ili kuondoa au kuzuia uwezekano wa kusababisha kero kwa wakaazi wengine wa eneo hilo;

(g) kupeleka mifugo katika majosho kama itakavyoagizwa na halmashauri;

(h) kupeleka mifugo katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(i) kuhakikisha mifugo inawekwa alama katika viungo vinavyopendekezwa;

(j) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri;

(k) kukusanya na kutupa taka zote zitokanazo na wanyama au ndege wafugwao katika maeneo maalumu ya kutupa taka;

(l) kuwa na eneo la kutosha kutunza wanyama hao, na kuhakikisha wanafungwa katika eneo la pamoja na si kuzurura ovyo; na

(m) kutokata miti ovyo.

Masharti ya mfugaji

31. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote-

(a) kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika mashamba au maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya kuchunga, kulishia na kunywesha mifugo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali cha Halmashauri;

(c) kuuza au kununua mifugo katika maeneo yasiyo ya mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri; na

(d) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo kinyume cha maelekezo ya Halmashauri.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

32. (1) Mifugo yoyote haitatakiwa kuzurura ovyo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Mifugo yoyote itakayokamatwa kwa kuzurura ovyo it

(3) Endapo mwenye mifugo atashindwa kulipa faini ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo kwa mnada mifugo hiyo, Mkurugenzi atatakiwa kukata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki zitarudishwa kwa mmiliki wa mifugo.

(5) Endapo mmiliki wa mifugo hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato vya Halmashauri.

(6) Endapo mwenye mifugo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri inaweza kurudisha fedha za mauzo ya mifugo hiyo.

(7) Halmashauri haitawajibika kwa gharama zozote enc

Ukaguzi wa mifugo

33. Halmashauri itafanya ukaguzi kwa kuingia katika nyumba, jengo au zizi lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba, jengo au zizi hilo.

Wajibu wa Halmashauri

34. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya-

(a) malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri; na
(b) njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi kutoka malishoni au minadani.

(2) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo.

Taratibu za kilimo

35. Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo zisizoharibu mazingira.

Masharti ya kilimo

36. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kulima katika miteremko, karibu au katika vyanzo vya maji au maeneo oevu yaliyotengwa, kandokando au kwenye kingo za mito, mabwawa na maziwa;

(b) kutumia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo kwa kufanya jambo jingine kinyume na kilimo;

(c) kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu cha maandishi kutoka kwa Halmashauri; au

(d) kufanya jambo lolote litakalohatarisha au

kuleta uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1)(c), muda utakaoruhusiwa kuchoma moto rafiki kwa mujibu wa kifungu hiki utakuwa ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi.

(3) Kwa lengo la usimamizi wa mazingira itakuwa ni

Matumizi ya viuatilifu

37. Halmashauri kwa kushirikiana na mamlaka husika za udhibiti wa viuatilifu zitaelekeza matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo, na kufanya ukaguzi ili kubaini viuatilifu ambavyo si rafiki kwa mazingira.

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI WA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

38. Halmashauri itawajibika kusimamia na kulinda vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka, alama na mabango ya ilani ya kuzuia uharibifu au uchafuzi katika maeneo hayo.

Kulinda eneo la hifadhi

39. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita sitini (60) toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti rafiki katika vyanzo vya maji.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

40. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 12, ni marufuku kwa mtu yeyote, kiwanda, taasisi, shirika kufanya jambo lolote ambalo litasababisha uchafunzi wa vyanzo vya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

Uchenjuaji wa madini

41. Ni marufuku kufanya shughuli za uchenjuaji wa madini au kuweka kitu chochote chenye sumu karibu au ndani ya chanzo cha maji au katika mito au maeneo mengine yanayotumiwa na binadamu au viumbe hai wengine.

## SEHEMU YA SITA
## HIFADHI YA MISITU

Uhifadhi wa uoto wa asili

42. (1) Kwa lengo la usimamizi wa mazingira Halmashauri zitawajibika kutenga na kuyatunza maeneo maalumu kwa ajili ya hifadhi za misitu, uoto wa asili na viumbe hai wengine.

(2) Endapo maeneo hayo yatakuwa yameharibiwa, Halmashauri itahakikisha kuwa inayarudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchomaji moto wa misitu

43.(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto msitu kwa namna yoyote ile.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kwa kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo kabla ya kusababisha madhara na uharibifu wa mazingira.

Kibali cha kuchoma moto rafiki

44. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto rafiki atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kwa majirani anaopakana nao kabla ya kuchoma moto katika eneo analokusudia na ataweka njia za kuzuia moto.

Ukataji wa miti

45. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti au kubangua magome katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa.

(2) Mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti kwa

matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi au shughuli nyinginezo ikiwemo kubangua magome atalazimika kupata kibali cha maandishi toka kwa Mtendaji wa Kijiji au kibali cha Afisa Maliasili wa Halmashauri au wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri.

(3) Kabla ya kutolewa kwa kibali cha kukata miti Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayotarajiwa kuvunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(4) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

Wachoma mkaa na kuni

46.(1)Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuchoma mkaa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) mtu yeyote anayetaka shughuli ya kuchoma mkaa au kukusanya kuni atatakiwa kupata kibali cha Halmashauri.

(3) Kibali cha Halmashauri kitatakiwa kuonyesha eneo na muda wa kufanya shughuli ya uchomaji na ukusanyaji wa kuni.

Wajibu wa kupanda miti

47. (1) Mtu yeyote, taasisi au asasi iliyoko katika Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kulingana na idadi itakayoelekezwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote anaweza kupanda miti katika shamba lake kadiri atakavyoona inafaa.

Siku ya kupanda miti

48. Kwa lengo la usimamizi na utunzaji wa mazingira Halmashauri itapanga siku maalumu kwa ajili ya kupanda miti.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

49. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote ambaye-

(a) ataingiza katika eneo la Halmashauri au atasafirisha

mifugo ndani au nje ya eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;

(d) atakiuka masharti ya kilimo kwa kulima katika miteremko, vyanzo vya maji, kingo za mito na maziwa, kutumia viuatilifu visivyoruhusiwa kisheria, au atafanya shughuli za kilimo katika maeneo ya malisho ya mifugo au eneo jingine lolote lisiloruhusiwa;

(e) atachimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(f) atatupa taka kwenye mitaro, barabarani, hifadhi ya barabara, vichaka au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(g) atashindwa kushiriki katika siku ya usafi na mazingira iliyopangwa na Halmashauri;

(h) ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;

(i) atachafua kwa namna yoyote au kuweka sumu, kemikali au madawa ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu na viumbe hai katika vyanzo vya maji au miundombinu ya maji;

(j) atachoma moto shamba bila kibali;

(k) atavuna mazao ya misitu bila kibali;

(l) atakata mti, atachoma mkaa, atakata kuni au kubangua magome ya miti bila kibali katika maeneo ya hifadhi au eneo lolote lisiloruhusiwa bila kibali

cha Halmashauri;

(m) atatupa taka ovyo, atatiririsha maji machafu, kuosha magari au mitambo au kufanya jambo jingine lolote linaloweza kusababisha kero, adha au chukizo kwa watu wengine au kuharibu mazingira;

(n) atamzuia afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake; au

(o) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii;

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii.

Adhabu

50. Mtu yeyote atakayetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

51. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa kumtoza kiasi kisichozidi shilingi laki mbili (200,000) baada ya kujaza fomu maalumu iliyoambatishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii

Tangazo la Serikali Namba 96 la Mwaka 2010

52. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 32(2))*

VIWANGO VYA FAINI KWA MIFUGO INAYOZURULA HOVYO.

| NA. | AINA YA MIFUGO | KIASI CHA FAINI KWA SIKU |
|---|---|---|
| | Ng'ombe | 5000 |
| | Mbuzi | 3000 |
| | Kondoo | 3000 |
| | Nguruwe | 4000 |
| | Mbwa | 2000 |
| | Ndege | 2000 |
| | Punda | 5000 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 51)*

## HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ......................................................................... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya....................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwamba tarehe ..........ya Mwezi ................... Mwaka................. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……. cha

Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ya Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……

Jina: ....................................................

Saini: ....................................................

Mbele ya:

Jina……...............................................

Cheo: ..................................................

Saini: ..................................................

Tarehe: .........................................

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye vikao husika vya kamati mbalimbali za Baraza la Madiwani lililofanyika tarehe 03/03/2018 na Mhuri huu ulibandikwa mbele ya:-

SEIF ALLY SAID
*Mwenyekiti wa )*
*Halmashauri ya Wilaya ya Pangani*

L.S

ISAYA MUGISHAGWE MBENJE
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Pangani*

NAKUBALI,

DODOMA,
03 Machi, 2020

SELEMANI JAFO,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*